



TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 31

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa Thelathini na Moja wa CRDB Bank Plc utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 16 Mei 2026, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba na kwa njia ya kidijitali kuanzia saa tatu kamili (Saa 3.00) asubuhi kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuridhia Dondoo.**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Thelathini uliopita.**
4. **Kujadili yatoakanayo na kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Thelathini.**
5. **Kujadili na kupokea Ripoti ya wenye dhamana ya Uongozi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2025.**

- 5.1 Ripoti ya wenye Dhamana ya Uongozi.
- 5.2 Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2025.
- 5.3 Gawio kwa mwaka 2025.

6. **Kuidhinisha Ada ya Wakurugenzi.**
7. **Kuteua Wakaguzi wa Hesabu.**
8. **Uteuzi wa Mjumbe mmoja huru wa Bodi.**
9. **Kujadili mapendekezo kutoka kwa Wanahisa.**
10. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
11. **Kupanga mahali na tarehe ya Mkutano ujao.**
12. **Kufunga Mkutano.**

MAELEZO

1. *Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 07/05/2026 na litafunguliwa tena tarehe 08/05/2026.*
2. *Mapendekezo kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 9 yatumwe na yamfikie Katibu kabla ya Alhamisi tarehe 07/05/2026 saa 10.00 jioni.*
3. *Kuanzia tarehe 04/05/2026, Kitabu cha Mkutano Mkuu kitapatikana matawini. Pia utaweza kupakua nakala ya kidijitali kwenye tovuti ya benki www.crdbbank.co.tz.*
4. *Taarifa ya fedha ya Mwaka 2025 itapatikana kwa njia ya kidijitali tu kupitia tovuti ya benki www.crdbbank.co.tz kuanzia tarehe 04/05/2026.*
5. *Wanahisa watakaohudhuria Mkutano Mkuu Arusha watajigharamia usafiri na malazi na kupokea kitabu cha Mkutano Mkuu kwenye ukumbi wa mkutano tarehe 16 Mei 2026.*

Kwa mawasiliano tumia anuani ifuatavyo:

Katibu

CRDB Bank Plc

S. L. P. 268

Dar-es-Salaam

Barua pepe: shares_unit@crdbbank.co.tz

Namba ya kiganjani: 0755 197 700

Namba ya WhatsApp: 0767 757 215

KWA IDHINI YA BODI

Pascal Mihayo

KATIBU

15 Aprili, 2026